# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO**

NSIMBO DISTRICT COUNCIL

## KIKAO CHA FINANCE CHA TAREHE 12/11/2021

**UMEANDALIWA NA KATIBU WA KAMATI LEONARD CHINJENGU**

Scanned with CamScanner

## HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA Mipango KUPITIA FEDHA ZA MIRADI YA UVIKO 19 PAMOJA NA KUBARIKI MATUMIZI YAKE CHA TAREHE 12/11/2021

**AGENDA**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUSOMA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO 19
3. KUAINISHA MIRADI AMBAYO FEDHA ZA UVIKO ZITATUMIKA
4. MAAZIMIO
5. MENGINEYO
6. KUFUNGA KIKAO

### 1. KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao muda wa Saa 3:15 Asubuhi kwa kutoa fursa ya kila mjumbe kujitambulisha na kisha kueleza agenda kuu ya kikao ambayo ni mapokezi ya fedah za UVIKO 19.

### 2. KUSOMA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO 19

Baada ya Katibu kusoma mapokezi ya fedha UVIKO 19, Mwenyekiti alianisha jumla ya kiasi kilichoingizwa katika Halmashauri Wilaya ya Nsimbo kuwa ni Tshs 2,159,445,822.51

### 3. KUAINISHA MIRADI AMBAYO FEDHA ZA UVIKO 19 ZITATUMIKA.

Mwenyekit alitoa Mchanganuo wa miradi ambayo itanufaika na fedha za UVIKO 19 kuwa miradi hiyo ni

(i) Shule za Msingi Shikizi
(ii) Shule za Sekondari Shikizi
(iii) Kituo cha afya Ugalla
(iv) Hospitali ya Wilaya ya Nsimbo
(v) Chanjo na vifaa tiba kwa ajili ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UVIKO 19

**ELIMU MSINGI**

Shule za Msingi ambazo zitanufaika na fedha hizi ni kama mchanganuo unavyo onekana hapo chini:-

(a) Mtambo -vyumba 7 vya Madarasa
(b) Kazaroho – vyumba 5 vya Madarasa
(c) Kamini – Vyumba 5 vya Madarasa

Scanned with CamScanner

(d) Sikwisi – Vyumba 5 vya Madarasa
(e) Imalamate- Vyumba 5 vya Madarasa
(f) Motomoto Vyumba 4 vya Madarasa
(g) Kalele - Vyumba 4 vya Madarasa
(h) Kasisi - Vyumba 3 vya Madarasa
(i) Kaloleni - Vyumba 2 vya Madarasa
(j) Jilabela - Vyumba 2 vya Madarasa
(k) Magula - Vyumba 2 vya Madarasa

Kila chumba kimoja kinagharimu Milioni 20 fedha za Kitanzania.

**ELIMU SEKONDARI**

Kwa upande wa shule za sekondari mchanganuo ni kama ifuatavyo.

(a) Sitalike – Madarasa 3
(b) Kenswa - Madarasa 2
(c) Katumba - Madarasa 2
(d) Kaburonge - Madarasa 2
(e) Itenka - Madarasa 5
(f) Nsimbo - Madarasa 5
(g) Ivungwe - Madarasa 5
(h) Uruwila - Madarasa 4
(i) Kanoge - Madarasa 4
(j) Ugalla River - Madarasa 4
(k) Mtapenda - Madarasa 4
(l) Machimboni - Madarasa 3

Kila darasa moja litagharimu Shilingi Milioni 20 za kitanzania

**AFYA**

Kwa upande wa sekta ya Afya fedha za UVIKO 19 zitatumika kugharamikia Miradi ifuatayo

(a) Nyumba ya watumishi 3 in 1
Nyumba hii itajengwa kituo cha afya Ugalla na itagharimu shilingi milioni 90 na itakuwa na uwezo wa kuchukuwa kaya 3 za watumishi kwa pamoja.

(b) Jengo la dharura la wagonjwa
Jengo hili litajenggwa katika hospitali ya Wilaya ya Nsimbo na litagharimu Tzs 300,000,000.00

Scanned with CamScanner

Mbali na utekelezaji wa miradi hii ya ujenzi fedha hizi za UVIKO 19 zitatumika pia katika kusambaza chanjo ya UVIKO 19 na gharama nyingine zitakazo kuwa sambamba na ugawaji wa chanjo hii

Fedha iliyotengwa na kutufikia kwa ajili ya shughuli za chanjo ya Uviko 19 ni Tzs. 29,345,882.5

## 4. MAAZIMIO

- Manunuzi yote yatumie Force Account kwa upande wa Mafundi ujenzi
- Manunuzi yote ya vifaa vya ujenzi yatatumia single source isipikuwa pale ambapo PMU itaona kuna haja ya kutumia njia nyingine
- Gharama za miradi ibaki kama muongozo wa Wizara unavyoonesha.
- Manunuzi ya vifaa vya ujenzi yaanze mara moja.
- Kamati mbalimbali za usimamizi wa miradi hii ziundwe haraka na baada tu kuundwa zianze majukumu yao mapema.

## 5. MENGINEYO

Hakuna

## 6. KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa kutoa Michango yao na kisha kufunga kikao mida ya saa nane Mchana.

............................
**MWENYEKITI**

............................
**KATIBU**

Scanned with CamScanner

| Kamati Finance | | 12/11/2021 | |
|---|---|---|---|
| 1. | Tabu Nzaw | DHRO | [illegible] |
| 2. | Joseph Asenga | DT | [illegible] |
| 3. | Victoria Andrea | DPLO | [illegible] |
| 4. | Malaka Morisho | DLO | [illegible] |
| 5. | Martin F. K | DE | [illegible] |
| 6. | Samora Katiri | EO | [illegible] |
| 07. | Revocatus R. Mapulo | D.O | [illegible] |
| 08. | John A Mgonga | DICTO | [illegible] |
| 09. | Helena D. Zangwe | DBU | [illegible] |
| 10 | Walokunga B. N | DHRO | [illegible] |
| 11 | Shengo PM | DAICO | [illegible] |
| 12 | Dr Ismail Kapwani | DMO | [illegible] |
| 13 | Leonard Chuyenga | CC | [illegible] |
| 14 | Muhabile Privatus | DEMO | [illegible] |
| 15. | Jonas M. Mwasyoke | DLNRO | [illegible] |
| 16 | Bahulia David | DIA | [illegible] |
| 17 | Elisongwo M. Mshiu | DSEO | [illegible] |

Scanned with CamScanner

# KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI

## ENEO: UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

**TAREHE: 15/11/2021**

**AGENDA:**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUSOMA MUHTASARI WA KIKAO CHA FINANCE CHA TAREHE 12/11/2021.
3. KURIDHIA NA KUPITISHA WASHINDI WA KAZI ZA UJENZI.
4. KURIDHIA NA KUPITISHA KOTESHENI ZA MANUNUZI YA VIFAA VYA UJENZI.
5. MENGINEYO
6. KUFUNGA KIKAO.

**1. KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao muda wa saa 4:15 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao

**2. KUSOMA MUHTASARI WA KIKAO CHA FINANCE CHA TAREHE 12/11/2021.**

Mwenyekiti alimnyanyua katibu wa bodi ya zabuni asome muhtasari wa kikoa cha finance cha tarehe 12/11/2021. Baada ya katibu kusoma muhtasari huu Mwenyekiti aliwaruhusu wajumbe kuchangia michango yao kwa kuzingatia maelekezo ya kikao hicho cha finance. Michango ya wajumbe baada ya kusomwa muhtasari huu ilikuwa kama ifuatavyo:-

a) Mjumbe 1: nashauri bodi iridhie manunuzi ya vifaa vya ujenzi katika miradi hii yafanyike kwa mujibu wa sharia za ununuzi na ugavi.

b) Mjumbe 2: ushindanishi wa kupata mafundi tuwaachie wakuu wa shule, walimu wakuu, waganga wafawidhi na serikali za vijiji, na taarifa zao za kutafuta mafundi ziwasilishwe ofisi ya PMU kabla ya tarehe 20/11/2021

c) Mjumbe 3: katika kutekeleza miradi hii ya UVIKO 19 maamuzi yote yafanywe ngazi ya Halmashauri.

d) Mjumbe 4: nashauri kipindi cha kutekeleza miradi hii ofisi ya ujenzi, manunuzi, mipango na idara zingine zitakazokuwa zinaonekana zinahusika kwa namna moja au nyingine zipewe taarifa juu ya ujenzi hu una washirikishwe kikamilifu.

Scanned with CamScanner

## 3. KURIDHIA NA KUPITISHA WASHINDI WA KAZI ZA UJENZI.

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe agenda hii ijadiliwe kwa kutoa maamuzi kama tunakubaliana na maamuzi yaliyofanyika ngazi za chini au tunakataa na maamuzi yalikuwa kama ifuatavyo:-

a) Washindi waliopatikana kupitiaa kamati za shule, vituo vya afya, wamepitishwa na tumewatunuku kazi walizoshinda kwa gharama walizojaza katika orodha ya mahitaji na bei walizopewa.

b) Mikataba ya washindi iandaliwe mapema kwa ngazi ya shule na kituo cha Afya.

c) Ofisi ya PMU isimamie upatikanaji wa fundi ujenzi kwa jengo la EMD

## 4. KURIDHIA NA KUPITISHA KOTESHENI ZA MANUNUZI YA VIFAA VYA UJENZI.

a) PMU iwaandalie kotesheni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi taasisi zote zilizopata mgao wa fedha za UVIKO 19

b) Manunuzi yote vifaa vya ujenzi yatasimamiwa na kamati zilizoundwa kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na serikali.

c) Manunuzi ya vifaa vya ujenzi jengo EMD yatasimamiwa na ofisi ya PMU

## 5. MENGINEYO

i. Idara zote zinazohusika kwa namna moja au nyingine katika miradi ya fedha za UVIKO 19 wawe wanahusishwa katika mienendo ya miradi hii.

ii. Nyaraka za kotesheni na mikataba ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi viwasilishe kwenye kikao kijacho cha bodi ya zabuni.

## 6. KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti alifunga kikao muda wa saa 8:40 mchana na kuwatakia wajumbe kuendelea na majukumu ya ujenzi wa Taifa katika idara zao.

Muhtasari huu umesainiwa na

Abdallah.

…………………………    …………………….

MWENYEKITI    KATIBU

Scanned with CamScanner

MAHUDHURIO

| NA | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | SAID MPUMBI | KAIMU M/KITI |
| 2. | SOLOMONI BOLDMAN | KAIMU HPMU |
| 3. | DR. ISMAIL KANANI | MJUMBE |
| 4. | VICTORIA ANDREW | MJUMBE |
| 5. | MALAKA MORISHO | MWALIKWA |
| 6. | ELISONGUO M. MSHIU | MWALIKWA |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

1. DANIEL WALAKUNGA — KWA TAARIFA
2. DANFORD SAGO — KWA TAARIFA
3. TABIA NZOA — KAIMU MKURUGENZI

Scanned with CamScanner